

**Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki**

**Huduma za Kijamii na Uhamishaji Makazi kwa ajili ya Bomba la  
Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Sehemu ya Tanzania**

**Mfumo wa Kisera wa Uhamishaji Makazi**

**Total East Africa Midstream BV**

**Septemba 2018**

Digby Wells  
Environmental

Warakaa huu umeandaliwa na Digby Wells Environmental

<b>Aina ya Ripoti:</b>	<b>Mfumo wa Kisera wa Uhamishaji Makazi</b>
<b>Jina la mradi:</b>	<b>Huduma za Kijamii na Uhamishaji Makazi kwa ajili ya Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki, Sehemu ya Tanzania</b>
<b>Msimbo wa Mradi</b>	<b>TOT4454</b>

<b>Jina</b>	<b>Muhusika</b>	<b>Saini</b>	<b>Tarehe</b>
Jan Perold	Mwandishi		4 Mei 2018
Grant Beringer	Mpitiaji		4 Mei 2018

Matoleo Toleo Namba	Marekebishtoleo	Tarehe ya ripoti
V1	Rasimu ya Mwisho ya iliyotolewa na Serikali ya Tanzania (GOT) kwa kipindi cha maoni	Mei 2018
V2	Toleo la RFP ya mwisho iliyotolewa kwa ajili ya kutoa taarifa zifuatazo maoni ya GOT	Septemba 2018

Ripoti hii inatolewa kwa madhumuni yaliyotajwa tu na haiwezi, kwa ujumla au sehemu yake, kutumika kwa madhumuni mengine yoyote bila ruhusa ya maandishi kutoka TEAM BV

## MUHTASARI

### **Maelezo ya jumla**

Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) ('Mradi') linahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba la mafuta liliofukiwa chini linalovuka mpaka kwa ajili ya kusafirisha mafuta ghafi kutoka Ziwa Albert nchini Uganda hadi pwani ya mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kuuza nje kwenye masoko ya kimataifa. Bomba hilo linaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, hadi kwenye Kituo cha kuhifadhia cha baharini (MST) huko Chongoleani, mkoani Tanga, Tanzania, kwenye pwani ya Afrika Mashariki. Urefu wa bomba ni kilomita 1,450, ambapo karibu kilomita 1,147 zitakuwa upande wa Tanzania. Bomba litavuka kutoka Uganda hadi Tanzania kwenye mji wa mpakani wa Mutukula. Bomba litavuka mikoa minane na wilaya 25 nchini Tanzania.

Total E&P Uganda B.V (TEPU), Tullow Uganda Operations Pty Ltd (TUOP) na CNOOC Uganda Limited (CUL) (Wabia wa Upstream) zina maslahi kwenye leseni za rasilimali mafuta karibu na Ziwa Albert, Uganda. Serikali ya Uganda na Serikali ya Tanzania, pamoja na Wabia wa Upstream, zinataka kujenga bomba hili kwa ajili ya usafirishaji nje ya nchi na miundombinu inayohusiana.

Ingawa njia ya bomba imechaguliwa ili kupunguza athari za mazingira na kijamii, uhamishaji wa vitu na makazi (upotevu wa makazi au kuhamishwa kwa kaya) na uhamishaji wa kiuchumi (upotevu, au kuzuia upatikanaji wa ardhi au rasilimali nyingine kwa ajili ya kuijilingizia kipato) kwa jamii hauepukiki na ardhi itahitajika kwa ajili ya vipengele mbalimbali vya Mradi.

Serikali za Uganda na Tanzania zilisaini Makubaliano ya Kiserikali (IGA) kwa ajili ya Mradi wa EACOP mnamo tarehe 26 Mei 2017. Makubaliano hayo yanaweka mfumo wa haki ardhi kwa Mradi uliokubaliwa na serikali, ikiwa ni pamoja na kuheshimu viwango vya kimataifa vya fedha. Hivyo upatikanaji wa ardhi na Mpango wa Mradi wa Uhamishaji utafanyika kwa mujibu wa mfumo wa kisheria wa Tanzania na viwango vya kimataifa (IGP), kama ilivyobainishwa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) Viwango vya Utendaji (PS) 5 kuhusu Upatikanaji wa Ardhi na Uhamishaji wa Lazima. Ikiwa mradi unajumuisha miradi mingine midogo au vipengele vingi ambavyo haziwezi kutambuliwa kabla ya uidhinishaji wa mradi, au ambavyo vinaweza kutekelezwa kwa mfululizo kwa muda mrefu, PS5 inaruhusu maandalizi ya awali ya Mfumo wa Kisera wa Uhamishaji (RPF) unaweka kanuni za jumla za mpango wa uhamishaji. Madhumuni ya RPF ni kuweka kanuni za upatikanaji wa ardhi, fidia na mpango wa uhamishaji, na ni kitangulizi cha RAPs na / au LRPs.

Mwaka 2013, Serikali za Tanzania na Uganda ziliidhinisha njia yeye upana wa kilomita 50, ambayo ilipunguzwa na kuwa kilomita 2 mwaka 2016 na mita 100 mapema mwaka 2017. Ndani ya mwaka 2017, njia hiyo ilipunguzwa hadi upana wa mita 30 ambapo njia ya kudumu itapita.

Ardhi kubwa katika eneo la Mradi inamiliwi kimila, na ardhi iliyosajiliwa au yeye hatimiliki ni ndogo hususani kwenye maeneo ya mijini (haipitiwi na njia ya bomba la mafuta). Uchumi wa mikoa inayoathirika na Mradi unategemea kilimo cha kujikimu na ufugaji wa mifugo. Pia kuna uchimbaji mdogo wa madini.

Mradi utahitaji kupata hekta 4,000 za ardhi. Sehemu kubwa ya ardhi hii (karibu 90%) inajumuisha ukanda wa ujenzi kwa bomba la mafuta kwa ajili ya kuuza nje. Makadirio ya mahitaji ya sasa ya ardhi ya Mradi yanaonyeshwa katika Jedwali ES 1-1.

#### **Jedwali ES 1-1 Makadirio ya Mahitaji ya Ardhi**

Kipengele cha Mradi	Makadirio ya Eneo Lililoathiriwa
<b>Miundombinu ya ujenzi</b>	
Kiwanda cha upigaji rangi / Eneo la mabomba (1 nchini Tanzania)	Hekta 40
Kambi kuu 2 za ujenzi pamoja na kituo cha reli	hekta 17.5 + hekta 18.0 = hekta 35.5
Kambi kuu 10 za ujenzi / Eneo la mabomba	Kati ya hekta 17.5 and hekta 18.4 takribani jumla ya hekta 175
<b>Ujenzi na Uendeshaji</b>	
Barabara mpya kwa ajili ya kufikia miundombinu ya ujenzi, njia ya bomba na miundombinu iliyo juu ya ardhi (AGIs)	Makadirio: hekta 74
<b>Miundombinu ya Uendeshaji</b>	
Bomba la kusafirishia nje ya nchi	
Njia ya ujenzi yeye upana wa mita 30	Upana wa njia: mita 30: hekta 3,441
Eneo la ziada la muda la ujenzi pembedi ya njia ya bomba (makadirio)	Hekta 163
Miundombinu ya kudumu AGI	
Kituo cha kuhifadhi cha baharini / Matenki	Hekta 72
Vituo vya pampu (vinajumuisha eneo la usalama, eneo la ujenzi, nk) (kila moja hekta 15.0 ambapo hekta 1.0 ni kwenye njia ya bomba)	Hekta 4 x 14 nje ya mita 30 za njia = hekta 56
Vituo 2 vya kupunguza msukumo (inakadiriwa hekta 3.3 kila ziada ya njia ya bomba)	Hekta 2 x 3.3 nje ya mita 30 za njia = hekta 6.6
Hifadhi ya Maji yaliyopimwa	Kuthibitshwa
Vituo vikuu vya valvu na vituo vidogo vya Umeme	Vitajengwa kwenye njia ya bomba, hakuna ardhi ya ziada inayohitajika
<b>Mahitaji ya jumla ya ardhi ya mradi (Ujenzi na Uendeshaji)</b>	<b>Hekta 4,063</b>

Hatua ya kwanza katika mchakato huo ni ujenzi wa miundombinu - makambi ya ujenzi na eneo la kuhifadhia mabomba, sehemu ya kupakia rangi, stesheni ya reli na barabara ujenzi. Katika waraka huu, "Maeneo ya Kipaumbele" hutumiwa kama neon la jumla kwa miundombinu hii, kwa kuwa miundombinu hii inatakiwa kujengwa kabla ya shughuli nyingine za ujenzi hazijaanza. Hii ni muhimu kwa ajili ya uhamishaji makazi, kwa kuwa ardhi kwa ajili ya Maeneo ya Kipaumbele inatakiwa ipatikane miezi kadhaa kabla ya maeneo mengine ya Mradi.

Kwenye mradi mkubwa kama huu wa bomba la mafuta, ujenzi hufanyika kwa wakati mmoja kwenye maeneo kadhaa kando ya njia ya bomba, ambapo wafanyakazi wa ujenzi kila mahali wanasonga mbele kwenye njia ya bomba la mafuta. Eneo linalojengwa na wafanyakazi wa ujenzi linajulikana kama "mtawanyiko". Mpango wa ujenzi wa bomba la mafuta utaamua idadi ya "mtawanyiko" inayotakiwa, kwa kuzingatia eneo la ardhi karibu na njia ya mwisho. Mara baada ya ujenzi wa EACOP kuanza utachukua takribani miezi 36.

Vikwazo vya kuingia kwenye eneo la Mradi wakati wa ujenzi vitawekwa kwa misingi ya kiafya na kiusalama. Ambapo baadhi ya vikwazo haviepukiki, sheria zitawekwa wakati wa ujenzi kwa ajili ya watu, magari na mifugo inayokatiza katika njia ya bomba la mafuta. Baada ya ujenzi na wakati wa awamu ya utekelezaji wa Mradi, mpangilio ya matumizi ya ardhi utakuwa kama ifuatayo:

- **Katika maeneo yaliyotengwa kama Kijiji kabla ya Mradi:** Eneo lote la mita 30 la njia ya bomba litapandwa nyasi. Hakuna maendeleo ya miundo, upandaji wa miti yenye mizizi mikubwa au shughuli za kilimo (k.m. uzalishaji wa mazao) utakaoruhusiwa. Hata hivyo mifugo, itaruhusiwa kuvuka na kula katika njia ya bomba;
- Katika maeneo yaliyotengwa kuwa Ardhi ya hifadhi na kuteuliwa kuwa eneo linalolindwa na / au teule (kwa mfano, hifadhi ya misitu, hifadhi ya wanyama, eneo la usimamizi wa wanyamapori, eneo la wanyamapori linalolindwa na eneo la wazi): eneo la ardhi litatunzwa na matumizi ya ardhi yatafanya kulingana na uwezo wa kibaiolojia. Hakuna ujenzi wa miundo au shughuli za kilimo (k.m. uzalishaji wa mazao) zitakazoruhusiwa katika njia ya bomba la mafuta, na hakuna miti yenye mizizi itakayopandwa kwenye mita 10 juu ya bomba la mafuta. Katika baadhi ya maeneo, mifugo haitaruhusiwa (k.m. katika baadhi ya Maeneo ya wanyamapori yanayolindwa) na kizuizi hiki kitaendelea baada ya ujenzi. Kwenye maeneo ambapo sasa mifugo inaruhusiwa kwenye hifadhi ya Ardhi, itaweza kukatiza na kula kwenye njia ya bomba la mafuta;
- **Kukatiza kwenye njia ya bomba la mafuta:** Wakati wa utekelezaji, Mradi utahitaji kufikika kwa bomba la mafuta wakati wote kwa ajili wa ukaguzi, matengenezo na ukarabati. Njia ya bomba la mafuta haitawekewa uzio na watembea kwa miguu na mifugo itaruhusiwa kukatiza. Magari machache yataruhusiwa kukatiza barabara na miundombinu iliyopo;

- **Miundombinu juu ya ardhi na MST itawekewa uzio:** Itawekewa uzio, na uingiaji wake utadhibitiwa kikamilifu

### **Mfumo wa Kisheria, Kisera na Kitaasisi**

Mradi utalazimika kukidhi mahitaji ya kisheria ya Tanzania kwa ajili ya upatikanaji wa ardhi, fidia na uhamishaji makazi pamoja na viwango vya kimataifa vya kifedha vinavyoendana na Kanuni za Ikweta (EPs) III na PSC za PSC.

Uchanganuzi wa tofauti ya sheria za kitaifa na viwango vya kimataifa na mikakati ya Mradi iliyopendekezwa utafanyika. Uchanganuzi utatoa taarifa kuhusu matakwa ya kisheria ya Tanzania na viwango vya IFC kuhusiana na uhamishaji makazi na fidia. Tofauti yoyote kati ya matakwa hayo, itashughulikiwa katika Muundo wa Stahiki utakapoandaliwa.

RFP inathibitisha kwamba, kunapokuwa na tofauti kati ya matakwa ya wakopeshaji (EPs na IFC PSs) na sheria za kitaifa, mfumo wenye nguvu zaidi utatumika.

### **Muktadha wa Kijamii na Kiuchumi na Matumizi ya Ardhi**

Bomba litapita katika mikoa minane kati ya 31 na Wilaya 25, angalia kielelezo ES 1-1

#### **Kielelezo ES 1-1: Njia ya bomba la mafuta na mikoa na wilaya itakayoathiriwa**

Eneo la Mradi kimsingi lipo kwenye ardhi ya vijiji. Uchanganuzi wa picha za satelaiti, unatofautisha kati ya makundi matatu ya ardhi katika eneo la mradi lililoathiriwa. Makundi haya ni:

- Kundi la 1- Ardhi inayotumika kwa kilimo (bila makazi ya kutosha);
- Kundi la 2 – Ardhi yenyе makazi pamoja na kilimo na / au malisho; na
- Kundi la 3 – Eneo la wazi au la ardhi ya makazi bila makazi na kilimo kwa kiasi kidogo.

Sehemu kubwa (takriban 55%) ya ardhi iliyoathirika na Mradi iko kwenye kundi la kwanza. Hali hii inaonekana katika mikoa miwili ya kaskazini iliyoathiriwa na Mradi (yaani Kagera na Geita, ambako takriban 50% ya ardhi iliyopitiwa na bomba la mafuta iko kwenye kundi la pili), pamoja na mkoa wa Manyara (ambapo sehemu kubwa ya ardhi iko katika kundi la tatu).

Maeneo kadhaa ya urithi wa kiutamaduni yapo kwenye njia ya bomba la mafuta, ikiwa ni pamoja na miti ya ibada, mapango, mawe ya tambiko na visima. Wakati wa mchakato wa kubuni njia ya bomba la mafuta, kulikuwa na uangalifu mkubwa ili kukwepa makaburi na maeneo muhimu ya kiutamaduni kadri yalivyobainika.

## **Uhamishaji – athari zinazohusiana**

Athari kuu zinazohusiana na uhamishaji wa makazi kutokana na Mradi ni kama ifuatavyo:

- **Uhamishaji wa makazi.** Inatarajia kwamba, kuna uwezekano mkubwa kujenga makazi mbadala mahali pengine kwenye ardhi hiyo hiyo. Kama haiwezekani, kaya zitahamishwa kwenye maeneo yanayofaa kwenye kijiji hicho hicho. Hivyo, inawezekana kwamba athari nyingi zinazohusiana na uhamishaji wa umbali mrefu zitaepukwa.
- **Upotevu wa miundombinu ya biashara.** Biashara ndogo ndogo ni shughuli za kawaida katika vijiji vingi nchini Tanzania. Kwa kawaida huwa katika muundo wa maduka au vibanda vya biashara, usagaji wa nafaka, saluni za nywele, mauzo ya mazao ya kilimo kwenye masoko ya nyumbani au vijijini, nk. Kuhamishwa kwa miundombinu inayokutumika kwa shughuli hizo za biashara kutasababisha uhamishaji kiuchumi, kwa kuwa itasababisha upotevu wa mapato kutokana na shughuli hizo mpaka miundombinu mbadala itakapojengwa mahali pengine.
- **Uhamishaji wa miundombinu ya kijamii.** Vijiji vingi vina miundombinu ya kijamii kama shule za msingi, makanisa moja au zaidi na / au msikiti, visima, ukumbi kwa ajili ya shughuli za kijamii, soko na kliniki au kituo cha afya. Wakati wa kubainisha njia ya bomba la mafuta, kulikuwa na uangalifu mkubwa ili kuepuka miundombinu ya kijamii kadri iwezekanavyo. Hata hivyo, kunaweza kuwa na uhamishaji mdogo wa miundombinu ya kijamii ambao hauwezi kuepukika kabisa.
- **Upotevu wa mashamba.** Upotevu wa mashamba yanayomilikiwa au kutumiwa na kaya unatarajiwa kuwa aina ya kawaida ya uhamishaji wa shughuli za kiuchumi kutokana na mradi. Uchanganuzi wa picha ya LIDAR ya njia ya bomba la mafuta unaonyesha kuwa sehemu kubwa ya Mradi itafanyika kwenye mashamba ya mazao.
- **Upotevu wa maliasili** Jamii karibu na eneo la Mradi hutegemea aina nyingi za maliasili: kuni za kupikia, mimea dawa, chakula (nyama ya porini, uvuvi), vifaa vya ujenzi nk. Usafishaji wa ardhi kwa ajili ya ujenzi itahusisha upotevu wa maliasili kama miti kwa ajili ya kuni au mbao, mimea inayotumiwa kwa ajili ya dawa, maeneo ya uwindaji, nk. Athari ya uchukuaji wa ardhi inayohusiana na Mradi kuhusiana na matumizi ya maliasili hizo itahusisha zaidi athari za upatikanaji (kwa mfano, uchepushaji) kwa kipindi mfupi wakati ujenzi (kwa mfano kwa jamii za upande mmoja wa njia ya bomba kutumia rasilimali za upande mwengine) kuliko kupoteza kabisa rasilimali. Makundi ya wawindaji-waokotaji matunda watakuwa katika hatari zaidi ya kuathirika. Vikwazo vyovyyote vya muda mfupi katika upatikanaji vinaweza pia kuathiri wafugaji, husasani ikiwa wana njia maalum ya kupita ili kuvifikia vyanzo vya maji na maeneo yaliyoteuliwa kwa ajili ya malisho. Athari hizi zinatarajiwa kuwa ndogo wakati wa awamu ya

uendeshaji wa Mradi, hata hivyo, maeneo yaliyochukuliwa na Mradi yana uwezekano wa kuwa sehemu ndogo ya maeneo yote ya ardhi ambapo rasilimali hizi zinapatikana.

- **Uharibifu wa barabara.** Njia ya bomba itakatiza idadi kubwa ya barabara za lami na changarawe. Katika hali ambapo barabara za kitaifa au mikoa hukatiza njia ya bomba, kutakuwa na athari za muda wakati wa ujenzi; hii inaweza kusababisha uchepushaji wa barabara. Haitarajiwu kwamba kutakuwa uharibifu wowote wa kudumu wa barabara utatokea. Inawezekana kwamba njia ya bomba inaweza kuathiri za maeneo husika au "zisizo rasmi" (miundombinu ya kijamii, biashara ndogo ndogo, nk) pia. Sheria zitawekwa wakati wa ujenzi na uendeshaji ili kuwawezesha watu, magari na mifugo kukatiza njia ya bomba, na hivyo kupunguza usumbufu wa ukosefu wa barabara. Hata hivyo, kwa kuwa njia ya bomba la mafuta haitawekewa uzio wakati wa awamu ya utekelezaji wa Mradi, haitarajiwu kutakuwa na vikwazo vikubwa kwenye miundombinu ya kijamii au maliasili (k.m. na jamii kwenye upande wa pili wa bomba).
- **Athari kwenye uchimbaji madini.** Viashiria vya sasa vinaonyesha njia ya bomba la mafuta linakatiza maeneo yenye haki ya ya utafutaji madini pamoja na maeneo ya madini ya wachimbaji wadogo yasiyoendeshwa kisheria. Maeneo haya yapo katika mikoa ya Geita, Shinyanga na Tabora.

Kwa ujumla, athari zinazohusiana na uhamishaji wa makazi ya mtu ye yeyote au kaya zinatarajiwu kuwa ndogo. Mbali na hali hii kwa ujumla:

- Uhamishaji wa ya makazi ya kaya (utakuwa sehemu ndogo ya jumla ya makazi ya kaya); na
- Watu ambao watapoteza sehemu au mashamba yao yote kwa ajili Mradi huu (pia inakadiriwa kuwa asilimia ndogo ya idadi ya kaya zitakazohamishwa).

### **Haki na Stahiki / Mfumo wa Malipo**

RPF inachukulia kwa umuhimu mkubwa suala la haki ya fidia na stahiki za uhamishaji. Haki, kwa madhumuni ya RPF hii, hutafsiriwa kama haki ya fidia na msaada unaotolewa kwa watu mmoja mmoja, makundi ya watu, familia, au taasisi kwa sababu ya uhamishaji makazi yao kwa ajili ya upatikanaji wa ardhi, uondoaji wa haki, na / au upatikanaji wa lazima wa ardhi ikiwa ni matokeo ya moja kwa moja ya Mradi.

Watu wanaohusika tu au kutumia eneo kabla ya tarehe tajwa (tarehe ya kwanza ya kuthaminisha eneo fulani) wanastahili kulipwa fidia kwa kupoteza haki za ardhi na mali zilizokuwepo kabla ya tarehe tajwa. Mali hizi tu zitarekodi wakati wa mchakato wa tathmini. Watu walioathiriwa wanapaswa kuwapo wakati wa mchakato wa tathmini, watu hao watatakiwa kutoa uthibitisho wa kuwepo kwao katika eneo la Mradi wakati wa tathmini, na / au ushahidi wa umiliki wa mali katika eneo la Mradi wakati huo, ili wastahili kulipwa fidia.

Mali zinazoathiriwa na Mradi zitafanyiwa tathmini kujua kiasi cha fidia watakacholipwa wamiliki na / au watumiaji. Njia ya tathmini itakayotumiwa inatajwa katika Sheria na Kanuni mbalimbali ambazo hutoa mwongozo kuhusu mchakato wa tathmini. Njia tofauti za tathmini zinapendekezwa kwa makundi mbalimbali yanayostahili kutambuliwa, hasa kuhusiana na ardhi, miundombinu, mazao, miti na biashara. Uchaguzi wa njia maalum ya tathmini utaendanan na matakwa ya kisheria ya Tanzania. Njia, chaguo na viwango vya tathmini, vinapendekezwa na Mradi ili kuhakikisha kwamba vigezo vya IFC PS5 vinashughulikiwa kikamilifu hususani "kuboresha au kurejesha shughuli za kujiingizia kipato na hali za maisha ya watu waliohamishwa kutoka kwenye makazi yao". Mambo muhimu katika suala hili ni pamoja na yafuatayo:

- Kanuni kuu ni kwamba mapendekezo ya Mradi ni kutoa fidia stahiki kwa ardhi iliyoathiriwa, ambapo Mradi unaathiri shughuli za kujiingizia kipato zinazofanyika kwenye ardhi na watu wanastahili, na mali zinaendana na IFC PS5;
- Watu wanaostahili watakaopoteza makazi yao na ardhi ya makazi watapewa fursa ya kuchagua kati ya fidia ya fedha na ujenzi mpya wa makazi. Nyumba mpya zitakazojengwa zitakidhi viwango vya ujenzi;
- Ikiwa miundo ya jumuiya (k.m., shule, vituo vya afya) itaondolewa, upotevu wake utafidiwa na na miundombinu mipyaa inayofaa;
- Watu wanaostahili wenye haki rasmi au za kimila za kumiliki ardhi ya kilimo watakaoathirika kwa kiasi kikubwa na Mradi watapewa uchaguzi kati ya fidia ya fedha au ardhi mbadala; na
- Mradi utaweka mpango wa kurejesha na kuboresha maisha ya watu walioathiriwa na Mradi (PAPs) na msaada wa kuandaa ardhi yoyote mbadala ya kilimo au kwa madhumuni yanayohusiana nayo.

Stahiki zinazohusiana na athari na wale walioathiriwa huwekwa katika RPF katika jedwali la stahiki.

### **Mchakato wa Uchukuaji wa Ardhi, Malipo ya Fidia na Uhamishaji makazi**

Mpango na utekelezaji wa uchukuaji wa ardhi, uhamishaji makazi na fidia kwa Mradi umeandaliwa kwa ajili ya kupata haki ya ardhi kwa ajili ya Mradi na kuhakikisha mchakato unaohusiana unaendana na sheria za Tanzania na viwango vya kimataifa vya fedha. Ardhi inahitajika kwa muda mfupi - kwa shughuli za ujenzi wa njia wakati wa ujenzi; na kwa muda mrefu - kwa ajili ya uendeshaji wa bomba, miundombinu ya juu ya ardhi, njia za kudumu na miundombinu ya mafuta ya baharini huko Chongoleani. Ardhi yote ya Mradi nchini Tanzania itachukuliwa kwa misingi ya kudumu, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu, na kisha itatolewa na Serikali kwa matumizi ya Mradi kwa mujibu wa kanuni za IGA.

Mchakato wa upatikanaji wa ardhi ya Mradi kwa muda mfupi na muda mrefu ni unaonyeshwa katika Kielelezo ES 1-2. Ardhi yote inayohitajika kwa ajili ya Mradi itachukuliwa kwa misingi kwamba Mradi huo ni kwa ajili ya maslahi ya umma na ardhi inayotakiwa kwa ajili ya Mradi itachukuliwa kwa maslahi ya umma, ambapo itatangazwa rasmi kwenye gazeti kwa mujibu wa masharti husika ya mfumo wa sheria wa Tanzania. Kampuni ya Mradi itakuwa na lengo la kufikia makubaliano ya fidia ya ardhi na mali zitakazoathiriwa na watu watakaoathirika na Mradi (PAPs). Endapo hili haliwezi kufikiwa na PAPs (au ikiwa hayapo) PAPs itatakiwa kuchukua za utekelezaji wa hatua zaidi za upatikanaji wa ardhi kwa lazima.

Utaratibu wa upatikanaji wa ardhi unasimamiwa katika awamu mbili kuu ambazo zinajumuisha shughuli kadhaa:

- Awamu ya shughuli za awali za upatikanaji wa ardhi ambayo inajumuisha uchunguzi wa kina na tathmini, na halafu ripoti ya tathmini (ambayo itakuwa na sehemu mbili - sehemu moja inayolenga kukidhi mahitaji ya kisheria ya Tanzania, na sehemu ya pili inayoonyesha stahiki za ziada ili kukidhi mahitaji ya IFC PS5); na
- Awamu ya upatikanaji wa ardhi na utoaji wa haki ambayo itasababisha upatikanaji wa ardhi na utoaji wa haki za ardhi kwa Mradi huu. Hii itahusisha utekelezaji unaofuata wa RAPs / LRPs, ikiwa ni pamoja na mikataba na PAP, malipo ya fidia, uhamishaji wa miundombinu, msaada wa kurejesha shughuli za kujingizia kipato, makubaliano ya mwisho ya haki za ardhi kuidhinishwa kwa Serikali na hati ya ardhi hii kutolewa kwa Kampuni ya Mradi.
- Utaratibu wa upatikanaji wa ardhi hatimaye utaishia katika suala la RAPs na / au LRP (baada ya uhamishaji wa miundombinu na shughuli za kiuchumi kufanyika). Eneo la kijiografia litakalohusika litabainishwa na mipaka ya utawala, na sehemu nyingine ni kutokana muda wa upatikanaji wa ardhi inayohitajika kwa vipengele mbalimbali vya Mradi. RAPs / LRP zinazopendekezwa zinajumuisha mambo yafuatayo:

RAP / LRP moja kwa maeneo ya kipaumbele, na RAPs nane / LRP kwa njia ya mabomba na AGI - imegawanywa kuzingatia maeneo ya kijiografia.

### **Kielelezo ES 1-2: Mchakato wa upatikanaji wa ardhi**

#### **Ushirikishwaji wa wadau**

Kampuni ya Mradi inatarajia kuwa na uhusiano wa muda mrefu, wa uwazi na wadau katika ngazi zote kama muhimu kwa shughuli zao. Kampuni ya Mradi imedhamiria kutoa taarifa, kushauriana na kufanya mazungumzoo kabla ya maamuzi yoyote muhimu kufanyika.

Inatarajiwa kutakuwa na vyombo kadhaa vya ushauri. Muundo na mamlaka ya vyombo vya ushauri iliyopendekezwa yatategemea majadiliano na, na idhini ya Serikali na wadau wengine

muhimu. Mambo haya yatakamilishwa wakati wa hatua za mwanzo za upangaji wa kina kama ifuatavyo:

- Kikundi Kazi cha Upatikanaji wa Ardhi na Uhamishaji (LARWG) kimeanzishwa kama chombo cha utawala na usimamizi kupitia kwake serikali ya kitaifa itashirikiana na Mradi kwenye masuala yanayohusiana na upatikanaji wa ardhi, fidia na uhamishaji. Chombo hiki cha kitaifa kinajumuisha wawakilishi kutoka Mradi wa EACOP, idara kuu za serikali na washauri elekezi wa makazi. Wawakilishi wa vyombo vingine vya serikali hushiriki kadri itakavyohitajika. LARWG inaongozwa na Serikali, lakini Kampuni ya Mradi inasaidia mchakato.
- Kampuni ya Mradi na timu ya RAP zitaendelea kushirikiana na kushauriana na mamlaka za serikali za mitaa katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Kata na Kijiji. Hii itajumuisha mikutano ya uhamashaji kabla ya kazi na shughuli zinazoendelea wakati wa kupanga uhamishaji na hatua za utekelezaji. Timu ya ushirikishaji wadau wa EACOP inajumuisha Maafisa Uhustiano wa Jamii ambao wapo katika mikoa minane itakayopitiwa na Mradi huo. Timu hii itaongezwa kadri Mradi unavyoendelea.
- Ushughulikiaji wa malalamiko utachukuliwa kama sehemu muhimu kwenye mchakato wa maendeleo ya RAP. Kuna mfumo uliopo wa ushughulikiaji wa malalamiko katika ngazi ya wilaya, ambapo wananchi wanaweza kulalamika kwa viongozi wa kata na / au wilaya. Mfumo wa kushughulikia malalamiko wa Mradi wa EACOP umeanzishwa na unasihamiwa na timu ya ushirikishaji wadau wa EACOP kupitia Maafisa wa Uhustiano wa Jamii. Mfumo maalum wa ushughulikiaji wa malalamiko umewekwa na unahusisha mifumo iliyopo.

### **Vipengele vikuu vya Bajeti ya uhamishaji**

Mwongozo wa maandalizi ya RAP au LRP unahitaji kila RAP au LRP kujumuisha makadirio ya bajeti ambayo itatumika katika utekelezaji wake. RPF inajumuisha maeleo ya taratibu za kufuata wakati wa upangiaji wa kina wa uhamishaji ili kuandaa makadirio ya bajeti ambayo yatajumuishwa katika RAPs au LRP.

Makadirio ya bajeti ya uhamishaji na urejeshaji wa shughuli za kujiingizia kipato hutegemea ukubwa wa athari za uhamishaji - idadi ya kaya zitakazohamishwa na kuathiriwa kiuchumi, nk. Ingawa makadirio ya ukubwa wa athari za uhamishaji yalitolewa katika FPR, tathmini ya athari itafanywa kulingana na tafiti zilizofanyika wakati wa kupanga uhamishaji. Makadirio mapya ya athari za uhamishaji yatatumika kwenye makadirio ya bajeti ya utekelezaji.

### **Muhtasari wa jedwali la stahiki**

Kama ilivyojadiliwa katika Sura ya 3 (uchanganuzi wa tofauti kwa ajili kulinganisha masharti ya wakopeshaji wa Kitanzania na wa Kimataifa), sheria ya Tanzania na IFC PS5 zote zinaruhusu

aina zote nne za stahiki; tofauti kati yao ni kwa kiwango cha msisitizo kinachowekwa kwa kila moja:

- Mahitaji ya Tanzania ni kwa kiasi kikubwa (lakini sio pekee) yanalenga fidia ya fedha; IFC PS5 inaruhusu fidia ya fedha, lakini inaonyesha kupendelea fidia isiyo ya fedha kwa masharti fulani;
- Sheria ya Tanzania inaruhusu aina mbalimbali za posho (posho ya usumbufu, posho ya malazi, nk); IFC PS5 inaruhusu posho fulani za ziada - k.m. posho ya mpito, posho kwa watu walio katika mazingira magumu;
- Sheria ya Tanzania inaruhusu fidia isiyo ya kifedha – hususani kwa ajili ya uhamishaji makazi; kama ilivyoelezwa, IFC PS5 inapendelea fidia isiyo ya kifedha; na
- Urejeshaji wa shughuli za kujiingizia kipato unategemea kukidhi matakwa ya IFC PS5; hata hivyo, kuna masharti fulani ya sheria nchini Tanzania ambayo yanataka kuwe na urejeshaji wa shughuli za kujiingizia kipato (k.m. upotevu wa Faida katika Sheria ya Ardhi).

Jedwali la 1- linaweka makundi mbalimbali ya upoteza wa faida unaotarajiwa, athari za upotevu, madhara ya kupoteza na stahiki. Mfumo wa Stahiki unataja stahiki kutokana na uwepo wa PAP stahiki na vitu vinavyoweza kulipwa kabla ya kuanza kwa mradi na stahiki zinaendana na IFC PS5.

## Jedwali1: Mfumo wa Stahiki

Athari		Matokeo	Watu wanaostahili	Stahiki
Ardhi	A1 Kupoteza Ardhi yenyenye makazi – ardhi yote inachukuliwa (kwa sababu yote iko kwenye sehemu ya Mradi au kwa sababu ardhi inayobaki inachukuliwa kama ardhi iliyoachwa na kwamba ardhi ya PAPS itaathiri shughuli za kujiingizia kipato	Uchukua (Upotevu wa kudumu)	Mmiliki wa ardhi Kimila, Na wamiliki wa ardhi kisheria Inatumika tu iwapo ardhi inachukuliwa kwa yote au inayobaki haitumiki.	<p><b>Malipo yasiyo ya fedha:</b></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Ardhi mbadala yenyenye ukubwa sawa na ardhi iliyopotea, katika eneo linalofaa, na usalama wa umiliki kwa mujibu wa IFC PS5;</li> <li>• Malipo ya gharama zote za manunuvi ;</li> <li>• Posho ya usumbufu;</li> <li>• Posho nyingine ikibidi; na</li> <li>• Kushiriki katika mipango ya kurejesha shughuli za kujiingizia kipato</li> </ul> <p>AU Malipo ya Fedha Taslimu:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Fidia (ikiwa ni stahiki) kwa upotevu wa kudumu wa ardhi kwa viwango vya soko kama ilivyolekezwa na Mtathmini aliyesajiliwa;</li> <li>• Posho kama hapo juu, na</li> <li>• Kushiriki katika program za kurejesha shughuli za kujiingizia kipato.</li> </ul> <p>AU Mchanganyiko:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>• Ardhi mbadala yenyenye ukubwa wa kawaida, mahali panapofaa, pamoja na usalama wa umiliki kwa mujibu wa IFC PS5;</li> <li>• Malipo ya fedha taslimu kama fidia kwa ardhi iliyoathiriwa na bila kupata ardhi mbadala (ikiwa ni stahiki);</li> <li>• Msaada wa mradi ili kupata ardhi kuchukua nafasi ya fidia ya fedha taslimu;</li> <li>• posho ya usumbufu;</li> <li>• Posho zingine ikibidi; na</li> <li>• Kushiriki katika program za kurejesha shughuli za kujiingizia kipato.</li> </ul>
	A2 Upotevu wa ardhi na makazi - sehemu tu ya ardhi inachukuliwa (na sehemu inayobaki inatumika kwa matumizi ya kiuchumi	Uchukuaji (Upotevu wa kudumu)	Mmiliki wa ardhi kimila na wamiliki wa ardhi kisheria	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Fedha taslimu zenye thamani sawa sehemu ya ardhi iliyoathirika;</li> <li>• Posho ya usumbufu;</li> <li>• Posho zingine ikibidi; na</li> <li>• Kushiriki katika program za kurejesha shughuli za kujiingizia kipato</li> </ul>

Kwa gharama ununuvi au usajili takwimu halisi zitapatika kutoka kwa mamlaka za eneo husika. 2 Kama inavyoleezwa Posho ya Usumbufu kwa mujibu wa sheria ni wastani wa kiwango cha asilimia ya riba inayotolewa na mabenki ya kibiashara kwenye amana za kudumu kwa miezi kumi na miwili ikiwa ni muda wa

kupoteza riba katika ardhi. 3 Hizi zinaweza kujumuisha gharama za benki zinazohusiana na taratibu za malipo ya fidia, kodi na gharama za manunuzi, pamoja na usaidizi wa mtaji wa awali, kama ni lazima. Hizi zitaelezwa na RAP. 4. Programu hizo zitatokana na matokeo ya utafiti wa masuala ya kijamii na kiuchumi na sensa ni sehemu ya mchakato wa RAP / LRP. 5. Ikibidi, mikopo ya nyumba inabadilishwa na kulipwa kwa taasisi ya mikopo. Kanuni hii inatumika kwa mali zote zinazohusiana na mikopo.

Athari	Matokeo	Watu wanaostahili	Stahiki
